

# MLINGANYO WA PENZI

James Kalekwa

# MLINGANYO
# WA
# PENZI.

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

SURA YA KWANZA....4
Penzi kama Hisia....4
Hisia ni zawadi....4
Hisia za Hasira....4
Hisia za Mapenzi....7
Hisia zina nguvu:....8
Mfano wa Hisia Kali za Mapenzi....11
Unafanya nini na Hisia zako?....13
Mfano wa Njaa ya Chakula....13
Hitimisho juu ya Upendo kama Hisia:....17
SURA YA PILI....18
Penzi kama Kanuni....18
Enendeni kwa roho....18
Sura ya Upendo....20
Hitimisho kuhusu Penzi kama kanuni....22
Kuhusu Mwandishi....23
Kuhusu New Vine Church:....23
Mawasiliano na Mwandishi....24

## UTANGULIZI:

Awali ya yote ninaomba nijitambulishe kwako ya kwamba mimi, mwandishi wa kitabu hiki ni kijana. Hivyo, ninaomba unisome kwa namna hiyo. Kwa vijana wenzangu mtakaosoma, nipokeeni hivyo. Usinione kama mzee aliyevuka hatua fulani. Na sasa amekuja kwa njia ya maandishi kuharamisha (demonize) hisia halali za ujana; au anawafokea vijana asioelewa nini kianendelea kwenye ulimwengu wao.

Ninaandika kama kijana niliyesaidiwa kwa namna ya ajabu na watu mbalimbali wa thamani. Kiasi kwamba huwa ninageuka nyuma na kusema laiti nisingekutana na watu wale; wasingenipa mafundisho; nisingesoma machapisho yao… hakuna namna ningekuwa hapa.

Kwa kitabu hiki ambacho ni mahususi kwa vijana wanaotafuta wenzi wa maisha na walio kwenye uchumba na hata wenye ndoa change (chini ya miaka mitatu). Ni kifaa mikononi mwako kuweka misingi imara sana ya mahusiano ya kimapenzi.

Kwa yeyote atakayesoma ambaye atadhani ujumbe hamuhusu sana. Tambua jambo hili ni hitaji halali (legit) kwetu vijana. Na sasa, twende wapi tukapate mafundisho isipokuwa kwenye kweli ya neno la Mungu?

# SURA YA KWANZA:

# Penzi kama Hisia

## Hisia ni zawadi:

Moja ya jambo tunapaswa kulitambua kwa yakini ni kwamba, Muumbaji, hana jambo alilolifanya kwa bahati mbaya. Kwa viumbe vyote alivyovifanya na ndani ya miili yetu wanadamu.

*“**Kila kitu amekifanya kizuri kwa wakati wake**; tena ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao; ili kwa jinsi mwanadamu asivyoweza kuivumbua kazi ya Mungu anayoifanya, tangu mwanzo hata mwisho.”* Mhubiri 3:11

Moja ya zawadi alizotupatia wanadamu ni hisia. Hivi ni vionjo vya ndani ambavyo baadhi huonekana nje kwenye mwili. Vionjo hivi, si bahati mbaya. Vinatumikia kusudi la Mungu. Vipo kutupatia taarifa fulani.

## Hisia za Hasira

Kwa mfano kionjo cha **hasira** ni hali ya ndani ya kutofurahia na kutokukubaliana na jambo fulani. Ni kweli kionjo hiki huwa kinaleta madhara mengi kama maandiko yasemavyo, *“Kwa maana hasira ya mwanadamu haiitendi haki ya Mungu.”* Yakobo

1:20. Neno limetuelekeza kuhusiana na hasira ya kwamba, *“Mwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka.”* **Waefeso 4:26**

Unaona, neno la Mungu linaelekeza namna ya kuenenda na kionjo hiki kiitwacho hasira. Iwepo lakini isipelekee kutenda dhambi.

Kionjo hiki unakihitaji sana kwenye maisha. Hususani ukijua wapi pa kukielekeza, muda gani wa kuelekeza kionjo cha hasira na kwa namna gani ya kuifunua hasira. Kwa mfano, maandiko yanaonyesha wapi hasira ielekezwe:

*“Pendo na lisiwe na unafiki* ***lichukieni lililo ovu****, mkiambatana na lililo jema.”* Warumi 12:9 Kama hujui kuchukia; kama hauna kabisa kionjo hiki. Wewe unapenda vyote. Kuna hatari ya kwamba hutachukia uovu. Lazima kionjo hiki kiwemo ndani yako.

*“Wala msishirikiane na matendo yasiyozaa ya giza, bali* ***myakemee****;”* Waefeso 5:11

Unaweza kukemea jambo jema? Unaweza ukakemea jambo linalokufurahisha? Unaweza ukakemea jambo unalopenda libaki kuwa lilivyo? HAPANA! Unakemea kile unachokichukia.

Dhambi siyo chakula kitamu; ni mauti – ni machinjio ya hatima nyingi. Inapaswa kuchukiwa kwa namna zote.

*"Enyi mmepndao BWANA,* ***uchukieni uovu****; Huwalinda nafsi zao watauwa wake, Na kuaokoa na mkono wa wasio haki."* Zaburi 97:10

Namna mojawapo ya kuufunua upendo ulionao kwa Mungu wako ni vile unavyouchukia uovu.

Maandiko yanaonyesha ni wapi si mahali sahihi pa kuelekeza kionjo hiki chema cha hasira, *"Bali yeye amchukiaye ndugu yake, yu katika giza, tena anakwenda katika giza, wala hajui aendako, kwa sababu giza imepofusha macho."* 1 Yohana 2:11

*"Kila amchukiaye ndugu yake ni mwuaji; nanyi mnajua ya kuwa kila mwuaji hana uzima wa milele ukikaa ndani yake."* 1 Yohana 3:15

> *"Kionjo hiki unakihitaji sana kwenye maisha. Hususani ukijua wapi pa kukielekeza, muda gani wa kuelekeza kionjo cha hasira na kwa namna gani ya kuifunua hasira."*

Kionjo cha hasira hakipaswi kuelekezwa kwa watu, hasa ndugu (jamii ya waamini). Biblia inaonyesha hasira haielekezwe kwa mwenzi wa maisha pia. Si lengo hasa la kitabu hiki kuliendea swala la hasira kwa mapana. Bali kutumia kama mfano wa vionjo vya kihisia.

## Hisia za Mapenzi

Biblia inaonyesha pia ya kwamba hisia ya kuvutiwa na mtu wa jinsia nyingine si shida. Bali unafanya nini na hiyo hisia ya upendo kumuelekea mtu wa jinsia nyingine ndiyo inaweza kuwa baraka au balaa.

*"17. Naye Lea macho yake yalikuwa dhaifu, lakini* ***Raheli alikuwa mzuri wa umbo, na mzuri wa uso.*** *18.* ***Yakobo akampenda Raheli****, akasema, Nitakutumikia miaka saba kwa kumpata Raheli, binti yako mdogo."* Mwanzo 29:17-18

Yakobo alivutiwa na Raheli; Biblia iko wazi kabisa juu ya sababu za kuvitiwa naye – uzuri wa umbo na uso! Unafanya nini na kuvutiwa huko, hilo ndilo jambo la msingi.

Sasa ni vizuri ukajua ya kwamba aliyeumba uzuri na mvuto ni Mungu wetu mwema mwenyewe.

*"Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa Kwa jinsi ya* ***ajabu na ya kutisha****. Matendo yako ni ya ajabu, Na nafsi yangu yajua sana."* Zaburi 139:14

Kuna vijana wa kiume ni wa ajabu na wa kutisha; kuna mabinti ni wa ajabu na wa kutisha! Isikusumbue, ndiyo utendaji wa Mungu wetu mwema.

Mungu ameweka vionjo vya pendo ndani yako; kuvutiwa na mtu fulani ili kukusaidia kwenye

kufanya machaguo na hatimaye kuhitimisha na kuendelea na maisha yanayofuatia. Iwapo hautakuwa mtu unayevutiwa; hautakuwa na hisia za kuvutiwa, utahangaika sana kwenye kufanya machaguo.

Kwa muda ambao nimehudumia vijana, nimekutana na vijana ambao hawavutiwi na aina yoyote ya mtu wa jinsia tofauti. Hivyo, wamemwachia Bwana wafanyie machaguo kisha awaletee. Wamekasimisha kwa Bwana swala la kionjo cha mapenzi. Watu wa namna hii huishia kwenye mahangaiko makubwa sana ya kimachaguo. Hata hivyo niligundua kuna baadhi si kwamba hawana kionjo hicho, lakini kwa sababu ya kuharamishwa (demonize) kihisia. Huwa wanavutiwa kisirisiri kiasi kwamba hawako radhi kusema kwa yeyote.

## Hisia zina nguvu:

Upendo kama hisia una nguvu ya kumwendesha mtu kwa namna nyingi sana. Neno la Mungu linamuonyesha mtu aliyezama kwenye hisia la lindi la upendo akitoa hitimisho kuhusu nguvu za hisia hizi.

*"Maji mengi hayawezi kuuzimisha upendo, wala mito haiwezi kuuzamisha; kama mtu angetoa badala ya upendo mali yote ya nyumbani mwake, Angedharauliwa kabisa."* Wimbo Uliobora 8:7

Si ajabu ukisoma kitabu hiki cha Wimbo uliobora utaona kibwagizo kinachojirudia mara tatu tofauti kuwaonya na kuwatahadharisha ambao muda haujafika na/au hawajajiandaa kuingia kwenye mahusiano ya kimapenzi *“Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, Kwa paa na kwa ayala wa porini, Msiyachochee mapenzi, wala kuyaamsha, Hata yatakapoona vema yenyewe.”* Wimbo Uliobora 2:7

Hii ni kuonyesha anajua nguvu yake na anawasaidia walio bado, wajiandae.

Vilevile maandiko yanafunua ya kwamba ukali wa hisia za upendo ni kama vile mtu aliyeko katika hali ya kuzimia… kwa lugha rahisi, hisia hizi ni kali kiasi cha mtu kupoteza fahamu. Si kwamba mwandishi anayakuza mambo (exaggerate), bali anaeleza uhalisia.

*“Nishibisheni zabibu, niburudisheni kwa mapera, Kwa maana nimezimia kwa mapenzi.”* Wimbo Uliobora 2:5

Hisia hizi za pendo ndizo zilimwangusha mnadhiri wa Mungu, mwamuzi Samsoni kwa Delila. Mbinu zote zilizotumika hazikuweza kumfikisha mahali pa kuelezea siri ya nguvu zake. Lakini *“mvinyo wa mapenzi”* moyo wake uliachia na misuli yake ililegea kiasi cha kusema siri iliyokuwa baina yake na Mungu.

*"Ikawa baada ya hayo* ***akampenda*** *mwanamke mmoja katika bonde la Soreki, jina lake akiitwa Delila. 13. Mwanamke akamwambia, Wawezaje kusema,* ***Nakupenda****; na moyo wako haupo pamoja nami? Umenidhihaki mara hizi tatu, wala hukuniambia asili ya nguvu zako nyingi. Ikawa, kwa vile alivyomsumbua kwa maneno yake kila siku, na kumwudhi,* ***roho yake ikadhikika hata kufa 17. Ndipo alipomwambia yote yaliyokuwa moyoni mwake,*** *akamwambia, Wembe haukupita juu ya kichwa changu kamwe...."* Waamuzi 16:4, 13-17

Kama kuna ushauri wa maana utawahi kupewa kwenye eneo la mapenzi ni huu: Usijidhanie una nguvu kiasi cha kupuuzia nguzu za hisia za mapenzi. Unaweza ukagundua nguvu ya hisia hizi baada ya kuwa zimekugharimu hatima yako kabisa.

Kama kilivyo kionjo cha hisia za hasira, ni baraka sana ikielekezwa inakotakiwa, kwa muda na namna inayotakiwa. Na kinyume chake huwa ni balaa na madhara yake ni makubwa sana. Ndivyo ilivyo hisia ya mapenzi, ni baraka na balaa, kulingana na wapi imeelekezwa, muda gani na kwa namna gani.

## Mfano wa Hisia Kali za Mapenzi:

Hapa ninataka walau kwa mfano mmoja kutoka kwenye maandiko, tuone muwako mkali wa hisia za mapenzi na matokeo yanayoweza kutokea.

*"Ikawa baada ya hayo, Absalomu, mwana wa Daudi, alikuwa na **umbu mzuri**, jina lake akiitwa Tamari, naye Amnoni, wama wa Daudi, **akampenda.**"* 2 Samweli 13:1

> *Usijidhanie una nguvu kiasi cha kupuuzia nguzu za hisia za mapenzi. Unaweza ukagundua nguvu ya hisia hizi baada ya kuwa zimekugharimu hatima yako kabisa.*

Unaona muunganiko wa uzuri wa Tamali na hisia za upendo za Amnoni? Amnoni hakuvutiwa na Tamari kutokea kusikojulikana... kulikuwa na uzuri (namna ya ajabu na ya kutisha iliyofanywa na BABA) ambao vionjo vya Amnoni vya pendo vilivutwa kuelekea. Ninataka uone ya kwamba hakuna ubaya katika kuvutiwa, bali unafanya nini baada ya kuvutiwa hilo ni swala la kujichunga nalo sana.

Sasa hizi hisia kali za upendo, kwa kuwa hakujua afanye nini nazo, zilianaza kuathiri mpaka afya na mwonekano wake, *"2. Akasononeka Amnoni, hata akaugua, kwa ajili ya umbu lake Tamari, maana huyu msichana alikuwa mwanamwari, Amnoni akaona ni vigumu kumtendea neno lo lote. 4. Naye*

*akamwambia, Kwa nini, Ee mwana wa mfalme, unakonda hivi siku kwa siku? Hutaki kuniambia? Amnoni akamwambia, Nampenda Tamari, umbu wa ndugu yangu, Absalomu."* 2 Samweli 13:2, 4. Hisia za penzi zilipelekea hali ya sonona (stress) kwa Amnoni na hatimaye hali ya mwili kukonda siku zilivyokuwa zikiendelea mbele.

Na hatimaye kutokea kwenye maandiko matakatifu, tunaona ya kwamba alizingatia ushauri wa rafiki yake, Yonadabu, akafanya udanganyifu kiasi cha kumpata Tamari kuja nyumbani/chumbani kwake. Hatimaye, alimtenza nguvu (alimbaka) (2 Samweli 13:5-14). Baada ya kuendeshwa na hisia zake, maandiko yanasema, *"Amnoni* ***akamchukia machukio makuu sana****; kwa kuwa machukio aliyomchukia yakawa makuu kuliko yale mapenzi aliyokuwa amempenda kwanza. Amnoni akamwambia,* ***ondoka, nenda zako****."* 2 Samweli 13:15

Matokeo ya tukio hili yaligharimu mahusiano ya Amnoni na Absalomu, hawakuzungumza kwa muda wa miaka miwili. Na hatimaye iligharimu maisha ya Amnoni na iliujeruhi pakubwa moyo wa Absalomu. Tafuta kitabu nilichoandika kiitwacho **Shujaa Aliyejeruhiwa**, utaona madhara kwa upana wake.

Ninataka uone upendo kama hisia ulivyo na nguvu ya kumuendesha mtu na kuleta madhara na

uharibifu mkubwa kiasi hiki. Iwapo hisia za upendoo zinaweza kuwa na athari kiasi hiki, swlai kubwa ni "**Ninafanya nini na hisia zangu**?"

## Unafanya nini na Hisia zako?

Kama kuna jambo ningependa lisondoke kwenye ufahamu wako ni hili, hisia za upendo ni baraka njema kutoka kwa Bwana. Kile unachofanya na hisia hizo ndicho hudhihirisha Baraka hiyo au huleta balaa. Kwa hiyo, usiziharamishe (demonize) hisia bali tambua nini unapaswa kufanya nazo ili upate matokeo aliyoyakusudia Mungu kwa kukupa zawadi hiyo.

### Mfano wa Njaa ya Chakula:

Njaa inaweza kutambulika katika ngazi mbili; kama hisia na kama hitaji la lazima la mwili. Njaa kama hitaji la lazima la mwili, ni ngazi ambapo mwili hauwezi kuendelea tena iwapo hautahudumiwa kwa chakula, *"Akafunga siku arobaini mchana na usiku, **mwisho akaona njaa**."* Mathayo 4:2 Hii ndiyo njaa kama hitaji la lazima la mwili.

Njaa kama hisia, ni kionjo ambacho kimewekwa na Mungu ndani yetu ili kiweze kuratibu (regulate) swala la ulaji na faida zake kwenye mwili wa mtu. Ukiachilia mbali swala la ulaji kwa ajili ya kuifurahisha nafsi, kimsingi ulaji ni kwa ajili ya

ujenzi wa mwili. Hebu fikiria kukiwa hakuna hii nguvu ya uratibu ndani ya mwanadamu; virutubisho vinavyotokana na chakula vitakosekana kwenye mwili wa mwanadamu. Kama watu kama mimi ambao kwao swala la kula ni kama "adhabu" huenda wangekula mara nne kwa mwaka mzima. Ukiondoa sababu za kufunga na mazoezi ya kinidhamu kuuweza mwili wako, kikanuni unapaswa kuitikia inavyotakikana nguvu hii ya uratibu (njaa) ili uvune matokeo mema kwenye mwili wako.

Ukiwa unahisi njaa, je ni halali kuvamia mghahawa na kujipakulia chakula chochote? Ukiwa na njaa unaruhusiwa kula kitu chochote unachokutana nacho ilimradi ushibe? La hasha! Huwezi kuchukua majani, udongo, chakula kibichi na kula ilimradi ukidhi njaa yako; Huwezi kuingia kwenye sehemu ya kuuza chakula na kujipakulia tu ili kuitikia kionjo cha njaa. Kuna utaratibu wa kufuata ili njaa iondolewe kwako. Ni kweli pia ya kwamba huwezi kuanza kulia na kupiga makelele hovyo ili watu waje kukidhi njaa yako. Pamoja na kwamba njaa uliyonayo ni hisia halisi na halali (valid) lakini inapaswa kutiririka kwenye utaratibu.

Akitokea mtu akachota tu mchele, akanywa unga, akavunja mayai na kunywa; au japokuwa hana fedha ya kulipia chakula cha mghahawa lakini akaamua kwenda kufanya fujo na kuvunja mghahawa ili

akidhi njaa yake… Hilo litatuashiria hali ya udhaifu wa kiakili wa mtu huyo. Hufanyi chochote tu eti kwa vile una njaa.

Na ndivyo ilivyo kwa hisia za upendo. Ni hisia za kweli na halali. Hata hivyo kile unachokifanya na hisia hizo, kinaonyesha afya ya utu wako wa ndani!

Mosi, amsha ufahamu juu ya mapenzi kabla ya mapenzi yenyewe:

*"Nawasihi, enyi binti za Yerusalemu, Kwa paa na kwa ayala wa porini,* ***Msiyachochee*** *mapenzi, wala* ***kuyaamsha****, Hata yatakapoona vema yenyewe."* Wimbo Uliobora 2:7

Mapenzi yako ndani ya kila kijana, na yamelala tu yakisubiri mapambazuko yake. Kuyachochea ni kuanza kuzilisha hisia za mwili zaidi kuliko kulisha ufahamu kuhisiana na eneo hili. Ni kuanza kuinua hamu za mapenzi. Inaweza kutendeka kwa kuona, kusikia, taswira za kifikra (imagination) na mazungumzo. Wakati kuyaamsha ni kuanza kushiriki matendo "madogo-madogo", hatua moja baada ya nyingine, ambayo muda si mrefu utajikuta kwenye madhara kama ya Amnoni.

Hisia zitakuja? Ndiyo – ni halisi na kweli. Zikusaidie kuelekeza machaguo (ought to inform your choices) na mwenendo wa swala hili. Lakini zitekelezwe ndani ya mipaka.

Pili, usienende nazo hovyo – kuna wajibu unaambatana na hisia za mapenzi.

Hisia za mapenzi zikiwekwa kwenye utendaji hazitakuacha bila wajibu. Ndiyo maana Mungu alifinyanga muundo ambamo hisia hizo zinapaswa kufurahiwa na wajibu wake kubebwa – huo ni mlinganyo mzuri sana. Huwezi kufurahia kwa uzuri hisia hizi ilihali ukikwepa wajibu unaoambatana nazo.

*"Mungu alifinyanga muundo ambamo hisia hizo zinapaswa kufurahiwa na wajibu wake kubebwa – huo ni mlinganyo mzuri sana. Huwezi kufurahia kwa uzuri hisia hizi ilihali ukikwepa wajibu unaoambatana nazo."*

Kwa habari ya Amnoni na hisia zake, Tamari alimsihi na kumuonyesha ya kwamba jambo analolitaka anastahili kulipata ikiwa atafuata utaratibu uliowekwa, *"...basi, sasa, nakusihi, useme na mfalme; kwa maana hatakukataza kunioa."* 2 Samweli 13:13. Amnoni hakusikia, akatenda kwa kuongozwa na hisia, akapata hasara ya maisha yake!

Ni vyema uanze kufahamu ya kwamba hisia za mapenzi zitakufikisha mahali ambapo utawajibika kwa mambo mengi ikiwamo, kuwaacha baba na mama yako (Mwanzo 2:24); kuwasahau watu wa nyumba ya baba yako (Zaburi 45:10) na kuambatana na mwenzi wako mmoja (Mwanzo 2:24). Kuna uzao

utakaotokea hapo ambao unawajibika kuufundisha mithili ya kocha (Mithali 22:6) na kuurithisha mali (Mithali 19:14).

## Hitimisho juu ya Upendo kama Hisia:

Hisia zote zinafanana tabia – huja na kuondoka; hupanda na kushuka. Si wakati wote maishani mwako huwa unakuwa kwenye hisia moja tu. La sivyo, maisha yasingekuwa na ladha. Hata hisia za penzi kumuelekea mtu fulani nyingine huja na kuondoka; hupanda na kushuka. Sasa, huwezi kuzitegemea kama chanzo thabiti cha maamuzi na msingi imara ya kujengea mahusiano ya penzi. Ndoa ikijengwa kwenye hisia, imegeukia uelekea wa machinjio yake tayari! Ndiyo, baraka ya hisia inatusaidia kuchonga muelekeo wa kupenda na kuvutiwa. Hata hivyo haipaswi kuachwa yenyewe tu ianze na kuendeleza ushirika wa wapendanao. Kuna kitu kikubwa kinapaswa kuja na kuweka mlinganyo (strike balance) kuanzia mwanzo mpaka mwendelezo wa kimapenzi.

Kama ilivyo kutembea ni *“kushoto-kulia”*; ndivyo ilivyo mapenzi hujengwa kwa hisia na kanuni! Sura inayofuatia inajielekeza kuangalia upendo wa kikanuni na kitabia ambao ni tofauti na ule wa kihisia. Huu ndiyo huleta uwiano kwenye mlinganyo wa penzi. Si uko tayari kujifunza?

# SURA YA PILI:

# Penzi kama Kanuni

Mungu aliyawekea maisha kanuni ili kuwe na uwezekano wa kutabiri matokeo kabla hayajatukia. Pia, iwapo kanuni zitazingatiwa kuwepo na uwezekano wa kurudiarudia matokeo maeneo mbalimbali, kwa wakati tofauti na watu tofauti. Ukiondoa kanuni kwenye maisha, yanakuwa ni vurugu. Ndivyo ilivyo kwa penzi, bila kanuni inakuwa ni fujo!

Baba yangu, askofu Goodluck Kyara aliwahi kunifundisha kuhusu kanuni na kuniambia ya kwamba, kanuni zipo ili zituwezeshe tuyafikie matokeo yanayoambatana na kanuni hizo. Wajibu wetu ni kuzipa kanuni ushirikiano na si kuzipinga. Kila anayejaribu kuvunja kanuni, basi huyo huvunjwa na kanuni.

Swala la penzi nalo limeundwa juu ya kanuni za kudumu.

## Enendeni kwa roho

*"16. Basi nasema, **Enendeni kwa Roho**, wala hamtatimiza kamwe tamaa za mwili. 18Lakini **mkiongozwa na Roho**, hampo chini ya sheria. 22. Lakini **tunda la Roho** ni upendo….."* Wagalatia 5:16, 18, 22

Ninataka uone kwa mkazo maalum hayo maneno matatu yaliyokolezwa wino “**Enendeni kwa Roho**”; “**Mkiongozwa na Roho**” na “**tunda la Roho**”**.** Unaiona nafasi ya Roho wa Mungu kwenye kuenenda kwako? Unaiona nafasi ya Roho Mtakatifu kwenye kuongozwa kwako na unaiona nafasi ya Roho Mtakatifu kwenye ujenzi tabia zitakazokupa kuenenda? Hizo tabi huitwa tunda la Roho na mojawapo ni upendo?

Ni vizuri ukafahamu ya kwamba mithili ya mtu anayetembea hawezi kwenda kwa mguu mmoja tu. Kutembea ni muunganiko wa hatua za mguu wa kushoto na wa kulia. Ndivyo ilivyo, upendo hisia ni mguu mmoja unaotakiwa kuwezeshwa na mguu wa pili uitwao upendo kanuni/tabia.

Tabia ya upendo, kwa mujibu wa maandiko, ni zao la uwepo na utendaji wa Roho Mtakatifu kwenye maisha ya mtu. Na hii ni tabia ambayo hupatikana kwa mwamini pekee. Tabia ni kubaki kwenye hali moja iliyosahihi kwenye mazingira na hali zote. Aina hii ya upendo haiamuliwi na mazingira, nyakati au mtu fulani. Huu ni upendo ambao unazalisha uwezo wa kufanya maamuzi thabiti, kuyasimamia na kuishi kwa hayo. Huo uwezesho unakuwemo ndani yako kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Kwa njia ya aina hii ya upendo unaweza kuamua kumpenda na kuambatana muda wote wa maisha na

mwenza uliyevutiwa naye. Huu ni upendo ambao haijalishi utakutana na watu wa jinsia nyingine walio wa namna ya ajabu na ya kutisha tofauti na mwenza wako, bado utabaki naye. Hutasema nimevutiwa na hawa zaidi kuliko yeye. Na ukweli unaopaswa kufahamika kwako ni kwamba, siku zote za maisha yako utakutana na wanadamu walioumbika kwa namna ya ajabu na ya kuitisha tofauti na mwenza wako. Na hilo ni Bwana asifiwe kabisa!

Kwa aina hii ya upendo hutafika mahali pa kusema "Sijisikii kumpenda tena" (I don't feel like I love him/her anymore). Mpenzi, siyo swala la ku-feel. Ni tunda la Roho.

Hakikisha umefika hapo ndiyo unyanyue miguu yako kuelekea stendi ya penzi. Kama bado, endelea kuandaa safari!

## Sura ya Upendo

Upendo ulitangazwa kwenye kitabu cha wagalatia kwamba ni tunda la Roho una mwenendo wake. Kwenye Maandiko Mtakatifu, kuna sura moja imejielekeza kuzungumzia mwonekano, tabia na matokeo ya upendo ikilinganishwa na mambo mengine yeyote.

Ninakuambatanishia hapa "The Love Chapter" ili uisome na uitumie kuupima upendo ulionao kumuhusu huyu mwenzi wako au atakayekuwa

mwenzi wako. Mimi na mke huiita hii sura kama "kipima pendo" chetu (love meter). Jikague na ukague upendo wako kwa kipimo cha surah ii.

*"1.Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao. 2. Tena nijapokuwa na unabii, na kujua siri zote na maarifa yote, nijapokuwa na imani timilifu kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, si kitu mimi. 3. Tena nikitoa mali zangu zote kuwalisha maskini, tena nikijitoa mwili wangu niungue moto, kama sina upendo, hainifaidii kitu. 4. Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; 5. haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya;6.haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli;7.huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote. 8. Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika. 9. Kwa maana tunafahamu kwa sehemu; na tunafanya unabii kwa sehemu; 10. lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika. 11. Nilipokuwa mtoto mchanga, nalisema kama mtoto mchanga, nalifahamu kama mtoto mchanga, nalifikiri kama mtoto mchanga; tokea hapo nilipokuwa mtu mzima, nimeyabatilisha mambo ya kitoto. 12. Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso; wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana. 13. Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo. (*1 Kor 13:1-13 SUV)

## Hitimisho kuhusu Penzi kama kanuni:

Bila kutumia miguu yote miwili ya penzi utajikuta umedondoka mahali fulani. Ama utakuwa uliyejaa msimamo wa kikanuni na hauna hisia zozote – itakupelekea kujitahidi au kujikaza badala ya kufurahia. Au utajikuta umefurishwa na hisia zilizojengwa hewani, madhara yake ni anguko la wakati wowote. Iwe ni kwenye ndoa, uchumba na/au urafiki unaoelekea kwe nye ndoa ya kiungu, tembelea miguu yote – cheza kwa miguu yote!

Kwa taarifa yako tu, penzi kama kanuni ndiyo litakuzuilia kuingia kwenye hali ya kumtenda dhambi Mungu katika jina la upendo. Pia, utashikiliwa dhidi ya jaribio la kumtenda hiyana mwenzi wa maisha yako.

Nimekuombea kwa Bwana Yesu ya kwamba maisha yako ya penzi yatakuwa kwenye mlingayo sahihi. Roho Mtakatifu akujaze hekima ya namna ya kuendea swala hili la penzi.

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: [https://www.newvinechurch.or.tz](https://www.newvinechurch.or.tz)

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Youtube: James Kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH *Dodoma*

# Abudu Nasi

**KILA JUMAPILI - saa 3.00 asbh -6.30 mch**

**KILA ALHAMISI - saa 11.00 jioni -12:15 jioni**



nvc_dodoma    +255 754 917 764

Mahali tulipo: **Swaswa - Njia Panda ya Waziri Mkuu**

*A Home of Impact*

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake; ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; Baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa
james_kalekwa
@MchungajiJK
+255 754 917 764